

**OFISI YA RAIS TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA  
SHULE YA SEKONDARI NGONGA  
S. L. P 272, KYELA- MBEYA.**

Email: ngongass2007@yahoo.com

Mob: 0784 516961, 0789145889, 0674139463

Kumb Na: KDC/S.3172/JI/2021

05/12/2020

Jina la Mwanafunzi \_\_\_\_\_

---

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI  
NGONGA WILAYA YA KYELA MKOA WA MBEYA MWAKA 2021**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza mwaka 2021** katika shule hii ya sekondari **Ngonga** ambayo ipo umbali wa **Km 8 Kusini** mwa makao makuu ya **Halmashauri ya wilaya Kyela**.

Muhula wa kwanza una anza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **05/01/2021** saa 1:30 asubuhi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **12/01/2020** Ndani ya siku saba. MZAZI/MLEZI  
UNAOMBWA KUFIKA TAREHE 03/01/2020 saa 3:00 asubuhi.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.**

**2.1 Sare za shule**

- a) Sare za shule hii ni Suruali Mbili (1) **kijani – dark green ( 2) Zambarau** kwa wavulana na Sketi mbili (1) **Kijani – Dark green( 2) Zambarau** kwa wasichana aina ya kitambaa imeambatanishwa. Na utatakiwa kuwa na T-shirt ya michezo ya rangi ya zambarau yenye kola (pia zinapatikana shuleni kwa Tshs. 10,000/=) kwa ajili ya siku za michezo na kazi maalumu.
- b) Aidha anatakiwa kuja na bunda lake la karatasi(ream paper) moja kwa ajili ya mitihani na majaribie ya wiki na mwezi, fedha haitapokelewa.

- c) Rangi ya hijabu ifanane na sare za shule
- d) Sare ya michezo kwa shule hii ni trakisuti (t-shirt na suluari) nyekundu kwa wavulana na wasichana t-shirt inapatikana hapa shuleni kwa bei ya tsh. 10,000.

## 2.2 Vifaa vingine vinavyo hitajika

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vifutavyo nyumbani ambavyo kila vitakapo hitajika atatakiwa kuleta shuleni kwa matumizi mbalimbali.

- (i) Jembe
- (ii) Ndoo
- (iii) Kwanja au panga

Vifaa hivi ni kwa ajili ya usafi na kazi za elimu ya kujitegemea.

## 2.3 Usafi

Mwanafunzi wakati wote anatakiwa kuwa safi kwa

- (i) Kuvaa nguo vizuri na nzuri, kutumbukiza shati ndani ya suluari au sketi (kuchomekea)
- (ii) Kunyoa nywele vizuri na kuzichana (sio za mtindo wowote ule) mitindo ya rasta, karikiti n.k hairuhusiwi upara au panki pia haviruhusiwi.
- (iii) Kuvaa mapambo kama vile mikufu, heleni, bangili, shanga, Kofia au kupaka rangi kucha, wanja, rangi za midomo, kuvaa pete n.k haviruhusiwi.
- (iv) Kufuga ndevu hairusiwi.

## **KUMBUKA**

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe uliyoambiwa kuripoti kwa ajili ya usajili na kuanza masomo. Kuchelewa kuripoti kutasabaisha kupoteza nafasi hii na kupewa mtu mwingine ambaye ana sifa.

## **3. Sheria na kanuni za shule.**

3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye

dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafutayo ambayo ni muhimu kwako ukiwa mwanafunzi katika shule hii.

- (a)heshima kwa walimu, viongozi,wazazi, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.
- (b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c)Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni kila siku (preparation)
- (d)Kuwa makini katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa
- (e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wa uanafunzi wako.
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

### **3.2 MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

- (i) wizi wa aina yoyote ile
- (iii) Uasherati, ubakaji, ulawiti, Ushoga
- (iv) Utumiaji, uuzaji, utangazaji, usambazaji au ubebaji wa dawa yoyote inayolevya mfano bangi, cocaine, pombe, kuber, mandrax, heroine na nyinginezo.
- (v)Makosa ya jinai
- (vi) Kupiga au kupigana, kutukana au kutukanana.
- (vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (viii) Kudharau bendera ya taifa.
- (ix) Kutoimba wimbo wa taifa.
- (x)Kuoau au kuolewa.
- (xi) Kuwa na mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- (xii) Kugoma adhabu, kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au wa mtu binafsi.

### **3.3. MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA YAFUATAYO;-**

- (i) kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe na yale ya  
Kulala wageni (Guest House), kumbi za kuonesha video.
- (ii) Kwenda nyumbani kwa Mwalimu au Mtumishi yoyote bila kibali  
Maalumu
- (iii) Kuingia ofisi za walimu, Maktaba, maabara bila kibali maalumu.

### **4. AGANO**

Ikiwa unakubali yote yaliyo andikwa humu ndani weka sahihi yako katika kiambata “A” mbele ya Mzazi/Mlezi wako.

**“EDUCATION SHAPE THE FUTURE”**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NGONGA.**

.....

**MOSES L. MWANGOMO**

**MKUU WA SHULE**